

»Mbolea minyoo ya maji maji: Dawa asili ya mimea «

Mbolea minyoo ya maji maji ni mbolea asili ambayo inaweza kuboresha rutuba ya udongo tena. Ni maji maji yanayokusanywa kutokana na maji yanayopitia kwenye mbolea ya mboji iliyotengenezwa na minyoo.

Mbolea hii ina vichocheo vya ukuaji, virutubisho ambavyo huhitajika na mimea katika viwango vidogo (virutubisho lishe), pamoja na virutubisho vivavyo huhitajika na mimea katika viwango vikubwa (virutubisho muhimu) kama vile nitrojeni, fosforasi na potasiamu. Mbolea hii huwekwa moja kwa moja kwa majani ya mimea ili kusababisha ukuaji wa haraka na pia gharama yake ni nafuu kuliko mbolea oza. Mbolea minyoo huongeza idadi ya viumbe hai wenyе faida kwenye udongo ambao husaidia mmea kunawiri. Pia inaboresha mimea bila kudhuru mazingira. Husaidia mimea na udongo kustahimili magonjwa na mashambulio ya wadudu. Ikilinganishwa na mbolea za kemikali, mbolea hii huongeza mazao na kupunguza gharama.

Kutengeneza mbolea minyoo ya majimaji

Mbolea minyoo ya maji maji hutengenezwa kwa pipa la plastiki la lita 100, na bomba. Kuzuia bomba kuziba, tumia vipande vidogo vya chandarua au kitambaa cha pamba kama kichungi. Weka pipa katika eneo lenye kivuli kwa sababu viumbe hai vyenye faida vilivyo kwenye mbolea minyoo ya maji maji vitakufa kwa joto kali. Jaza pipa na cm 10 hadi 15 ya majani makavu, kisha ongeza kiasi sawiya cha majani ya mpunga, na kilo 5 hadi 10 ya samadi ya ng'ombe iliyooza. Ongeza 2kg ambazo ni sawa na minyoo 2000 ndani ya pipa. Ongeza lita 2 hadi 4 za maji kwa upole ili kuepuka kuwadhuru minyoo. Funika pipa kwa kitambaa ili kuepuka minyoo kushambuliwa na mchwa.

Mchanganyiko na usimamizi

Baada ya siku 10, mbolea minyoo ya maji maji huanza hujitengeneza kwenye pipa. Kila siku, unaweza kukusanya lita 1 hadi 3 za mbolea minyoo ya maji maji kutumia bomba. Mbolea minyoo ya maji maji ambayo ni bora ina rangi ya hudhurungi na inaweza kuhifadhiwa hadi miezi 6. Ongeza lita 1 ya mbolea minyoo ya maji maji kwa lita 10 za maji. Mkojo unaweza pia kuongezwa kwa mbolea minyoo ya maji maji kwa sababu mkojo hufanya kama dawa ya kuvu. Nyunyiza mchanganyiko wa mbolea minyoo ya maji maji wakati mimea inapochana maua. Nyunyiza mimea asubuhi mapema au jioni ili kuepusha joto kuyeyusha mbolea.

Mbolea minyoo ya maji maji pia inaweza kutumika katika umwagiliaji wa matone. Unaweza pia kulowesha mizizi ya miche kwenye mbolea minyoo ya maji maji kabla ya kupandikiza miche, na hivyo mizizi itakuwa yenye nguvu na afya. . Mbolea minyoo ya maji maji inaweza kunyonyizwa kwenye udongo kabla ya kupandikiza miche ili kudhibiti wadudu.